OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA KILOSA

KIDETE DAY SEKONDARI,
S.L.P. 71,
KILOSA.

KUMB. NA. KSS/4316/KDT I/2021 10/12/2020

.....
S.L.P ..170.....
KILOSA.

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KIDETE DAY, WILAYA YA KILOSA, MKOA WA MOROGORO MWAKA 2020.

1:0 **UTANGULIZI**

Ninayofuraha kukutaarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha KWANZA katika shule ya sekondari KIDETE DAY. Shule hii ipo umbali wa Kilomita 82 kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa kupitia barabara ya Lumuma. Shule ipo Makao makuu ya Kata jirani na kituo cha Stesheni ya Reli.

Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe 11/01/2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 29/01/2021.

Kutoripoti shuleni ni kosa kisheria, hatua kali za kisheria zitachukuliwa kwa mzazi/mlezi ambaye hatomleta mtoto wake.

2:0 **MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

A: SARE ZA SHULE

(i) **WAVULANA**

- Suruali mbili (2) pana zenye rinda mbili za rangi ya kijani na shati mbili (2) nyeupe za tomato zenye mikono mifupi.
- Viatu vyeusi vya ngozi (SIO RABA) vyenye kamba.
- Soksi nyeupe.
- Mkanda mweusi wenye kichuma cha kawaida cha kufungia.
- Sweta la kijani

(ii) **WASICHANA**

- Sketi mbili za rangi ya kijani mshono wake uwe wa linda box ndefu kupita magoti na zisizobana.
- Soksi nyeupe.
- Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba na visivyo na visigino virefu.

Scanned with CamScanner

- Hijabu ndefu na nusu kanzu kwa wanafunzi wa kike wa kiislamu.

B: SARE ZA MICHEZO

- T.Shirt ya rangi ya Blue kwa wasichana na wavulana.
- Bukta ya Blue
- Tracksuti ya blue kwa wasichana.

C: VIFAA VYA KUJIFUNZIA

- Madaftari makubwa (counter book Quire 2 au zaidi) yawe 11.
- Mkebe wa hesabu (Mathematical set)
- Kalamu za wino (Blue or Black za kutosha)
- Begi la kubebea vifaa vyake **(Kumbuka siyo mfuko)**

2.1: **VIFAA VYA USAFI SHULENI**

Njoo na vifaa vifuatavyo kwa ajili ya kufanyia usafi shuleni

- Ufagio wa chelewa
- Ndoo ndogo ya lita kumi
- Mti mmoja wa kupanda shuleni ni lazima kwa kila mwanafunzi.

KUMBUKA

Kwa vifaa vya usafi ni Agizo la Bodi ya shule katika kikao chake cha tarehe 09/12/2020 pamoja na makubaliano ya vikao vya wazazi. Aidha hatupokei **FEDHA** yoyote shuleni kwa ajili ya vifaa hivyo.

3:0 **SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII NI:**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu No. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyolekebishwa kwa sheria No. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu Sayansi na teknolojia yenye dhamana ya Elimu chini na ofisi ya Rais Tamisemi yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu.

Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

(a) Heshima kwa viongozi, walimu, wazazi, wanafunzi wengine, wafanyakazi wote na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima

(c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation)

(d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.

(e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uwanafunzi wako katika shule hii.

(f) Kutunza usafi wa mwili na malazi na mazingira ya shule

Scanned with CamScanner

(g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
(h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na
(i) Kutunza mali za Umma.

3:2 **MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA UFUKUZWE SHULE**

(a) Wizi wa aina yeyote ile
(b) Uasherati, ubakaji, usagaji na ushoga
(c) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya
(d) Uvutaji wa sigara na bangi
(e) Makosa ya jinai
(f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
(g) Kudharau Bendera ya Taifa
(h) Kuoa au kuolewa
(i) Kupata mimba, kutoa mimba, kusababisha au kushawishi kutoa mimba
(j) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
(k) Kukataa adhabu kwa makusudi
(l) Kuwa na simu ya mkononi

4:0 **MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA NA MWANAFUNZI SHULENI**

(a) Medical examination form ambayo itajazwa na Mganga mkuu wa hospitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.
(b) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

Tafadhali soma kwa umakini maelekezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

"ELIMU KWA MABADILIKO"
KIDETE DAY BILA ZIRO INAWEZEKANA

.....
KING'ARE M. SILAS
MKUU WA SHULE

Scanned with CamScanner

APLNDLX C: MEDICAL EXAMINATION FORM

SHULE YA SEKONDARI KIDETE DAY
S.L.P 71 KILOSA
Email: kideteday3hm@yahoo.com
Mob.....
Date...../...../.....

PART A:

Mr./miss.....

Please examine the above named student as to his/her physical and mental fitness for full time student in this school. The examination should include the following:

1. Hemoglobin.....
2. P V bleeding.....
3. Sight.....
4. Blood pressure.....
5. Urine for sugar.....
6. Stool for routine examination.....
7. Pregnancy test.....
8. Skin diseases.....
9. Leprosy.....
10. Any deformity.....
11. Epilepsy.....
12. Pulmonary tuberculosis.....
13. Neurosis.....
14. Venereal diseases.....
15. Other serious diseases.....

PART B.

(To be completed by Government Medical Officer)

1. I have examined the above named student and consider that he/she is Physically fit/unfit for a full time schooling.
2. Other Comments:

   .....

   .....
3. Date...../...../..... signature.....

   Station..... Designation.....

   Official stamps.....

Scanned with CamScanner

KIAMBATANISHO A: FOMU YA KUMUANDIKISHA MWANAFUNZI SHULENI
OFISI YA RAIS UTUMISHI, TAMISEMI NA UTAWA BORA

SHULE YA SEKONDARI KIDETE DAY

(Jaza fomu hii kwa uangalifu)

Picha ya mwanafunzi

1. Jina kamili la mwanafunzi.....

2. Tarehe ya kuzaliwa...../...../.....wilaya.....

3. Kabila.....urala.....dini.....

4. Jina la mzazi.....

Anuani ya mzazi.....

Kazi ya mzazi.....simu na. .....

(Sehemu hii ijazwe na wanafunzi ambao hawakai na wazazi wao YAANI YATIMA)

5. a. Jina la mlezi.....

b. Uhusiano kati ya mlezi na mwanafunzi.....

c. Kazi ya mlezi..... Simu na.....

d. Anuani ya mlezi.....

6. Shule atokayo mwanafunzi.....

7. Wakati wa likizo mwanafunzi atakwenda wapi? .....

8.Maelezo ya mwanafunzi:

.....

.....

9. Ujuzi/stadi nyingine.....

Sahihi ya mwanafunzi ..... Tarehe...../...../.....

KIDETE SECONDARY

Scanned with CamScanner

KIAMBATANISHO A: FOMU YA KUMUANDIKISHA MWANAFUNZI SHULENI

OFISI YA RAIS UTUMISHI, TAMISEMI NA UTAWA BORA

SHULE YA SEKONDARI KIDETE DAY

Mimi ..... msichana/mvulana ninakubali kulngia kidato cha ..... katika shule ya sekondari KIDETE DAY

Kama mwanafunzi wa kutwa/bweni tarehe...../...../..... Nitafika shuleni bila kuchelewa. Nitatii sheria za shule na nitaishi maisha mazuri. Nitakuwa mwanafunzi mwenye bidii katiaka masomo na kazi za kujitegemea, nitalazimika kulipa uhalibifu wowote uwe ni majengo,vitabu na vitu vyote nitakavyoharibu nikiwa shuleni ama nje ya shule.

Sahihi ya mwanafunzi..... Tarehe...../...../.....

SEHEMU YA MZAZI/MLEZI:

Mimi ..... Ninakubali mtoto wangu.....asome katika shule ya sekondari KIDETE DAY kuanzia tarehe...../...../..... ninahaidi kumpatia vitu vyote anavyotakiwa kuwa navyo shuleni kama ilivyotajwa katika barua.

Ninakuhakikishia kwamba nitamwonya mtoto wangu kutii sheria za shule na kuishi maisha mazuri na kuwa na bidii kwenye masomo na kazi za kujitegemea.

Ninakubali kuwa mtoto wangu amekubali kuingia katika shule ya sekondari KIDETE DAY kama mwanafunzi wa kutwa/bwen. Hivyo muda wa mwanafunzi kuwa shuleni ni saa moja kamili asubuhi hadi saa tisa na nusu mchana, na nitawajibika kwa malezi ya ziada kwa muda ambao si wa masomo na siku za mapumziko.

Anuani yangu ya kudumu ni:

.....

Sahihi.....tarehe...../...../.....

KIDETE DAY SECONDARY

Scanned with CamScanner